

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUKOMBE

MKOA WA GEITA

Simu:0282520709

Barua pepe: ded@bukombedc.go.tz

Tovuti: www.bukombedc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

S.L.P 02,

Ushirombo

BUKOMBE

TAARIFA KWA UMMA.

Jumla ya wanafunzi 5,073 wanatarajiwa kuanza mitihani yao ya kumaliza elimu ya darasa la saba (7) ambayo itafanyika kuanzia Tarehe 05 Septemba siku ya Jumatano na kumalizika tarehe 06 Septemba 2018.

Watahiniwa 5,018 ni wa shule za serikali ambapo wavulana (ME) 2,428 na wasichana (KE) 2,590, na Watahiniwa wa shule binafsi (55), wavulana (ME) 29 na Wasichana (KE) 26.

Kwa Kipindi hiki cha mwaka 2018 idadi ya watahiniwa imeongezeka kutoka watahiniwa 4,601 mwaka jana 2017 hadi watahiniwa 5,018 mwaka huu 2018 kutokana na usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa Kamati KUU ya Wilaya na Afisa Elimu wa Wilaya Ndugu Shadrack Kabanga katika kudhibiti utoro na mimba shulenii.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe Ndugu Dionis Myinga anawatakiwanza wanafunzi wote mitihani mema, kuwa watulivu, kufuata sheria na taratibu za Mitihani.

Pia ameomba wazazi kuendelea kuwaombea na kuwapa moyo watoto ili wafanye vizuri katika Mitihani yao.

KILA LA KHERI WANAFUNZI WOTE WA DARASA LA SABA WILAYANI BUKOMBE 2018.

Imetolewa Na;

Tusa D Mwambenga

Afisa Habari

BUKOMBE

04/09/2018